Shalom, karibu tujifunze Neno la Mungu. Biblia inatuambia..

> *“Ondoa takataka katika fedha, Na chombo kitatokea kwa mtakasaji; (Mithali 25:4)*

Tunapoiona dhahabu au madini mengine yote, yanang’aa sana, mpaka kufikia kiwango cha kuuzwa kwa thamani kubwa sana, hatupaswi kudhani, huko chini yanapochimbwa yanatoka kama yalivyo. Hapana, mengi ya hayo yanakuwa yamechanganyikana na mawe mengine au uchafu mwingi tofauti tofauti, kiasi kwamba unaweza kukutana na mwamba mkubwa sana, na ndani yake kukawa na kiwango kidogo sana cha dhahabu au fedha.

Hivyo, ili kuipata dhahabu yenyewe safi, inawagharimu wafuaji wafanye kazi ya ziada, na kazi yenyewe ndio hiyo ya kutenganisha madini hayo kutoka katika hizo takataka nyingine, Zipo takataka ambazo unaweza kuziondoka kwa kuzichuja tu au kupepeta, lakini zipo ambazo itakuhitaji utumie moto ili kuzitenganisha, kwasababu inakuwa zimechanganyikana na dini lenyewe hadi ndani.

Hivyo wanachokifanya ni kwenda kuyachoma mawe hayo, kwa joto kali sana mpaka yayeyuke, na yakishayeyuka na kuwa kama uji uji,  ndipo sasa uchafu unajitenga na dhahabu yenyewe.  Kwa kupanda juu, hapo ndipo yule mfuaji anapoondoa uchafu ule,  na atarudia tena hizo hizo hatua kwa jinsi atakavyoweza, na kwa jinsi atakavyozidi kuondoa takataka hizo zote hata zile ndogo, ndivyo, mnga'o wa fedha hiyo unavyozidi kuja.. hatimaye, inatokea ikiwa nzuri sana yenye kupendeza, tayari kwa matumizi yenye thamani.

> *Mithali 25:4 "Ondoa takataka katika fedha, Na chombo kitatokea kwa mtakasaji;".*

Hivyo na sisi pia kama wakristo, tunapookoka tunakuwa hatuna tofauti na fedha/dhahabu iliyochimbwa katikati ya miamba, tumetolewa huko tukiwa na mambo mengi ya kidunia  ambayo yameshikamana sana na sisi,

Sasa tunapookoka, kanuni ni ile ile inatugharimu tuingizwe katika moto, ili tuwe safi kabisa, Na moto huo anayetuingiza ni Mungu, na pia tunajiingiza sisi wenyewe.

Hapo ndipo utaona pale tunapokuwa wakristo tu, Mungu anaruhusu tupitishwe katika majaribu mbali mbali ya moto ili tuwekwe safi. Ndio maana biblia inasema;

> *1Petro 1:6 "Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali;*
>
> *7 ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo".*

> *Yakobo 1:2 "Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali;*
>
> *3 mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi".*

Unaona, ni jambo la kawaida Mungu, kuwapitisha watoto wake

katika majaribu ya namna mbalimbali, lengo sio kuwaangamiza, bali kuwaimarisha Zaidi.

Pia Neno la Mungu linatuambia na sisi wenyewe, tunapaswa tuondoe takataka katikati ya kila kitu tunachokifanya katika maisha yetu ya ukristo ili Mungu aweze kutufanya kama vile anavyotaka, iwe ni katika  huduma zetu, au  shughuli zetu n.k..

Tukitaka tumwone Mungu katikati ya Maisha yetu, tuondoe mambo ambayo hayampendezi, tuondoe uzinzi, tuondoe usengenyaji, tuondoe kuchat chati kusikokuwa na maana mitandaoni, na kutazama muvi muvi zisizotujenga, tuondoe mizaha, tuondoe unafki, tuondoe rushwa, tuondoe uvaaji mbovu, n.k. Mambo kama haya tukiyazingatia basi Mungu, atatuletea ule mng'ao tunaostahili kuwa nao sisi kama wakristo, na tutakuwa wa thamani nyingi mbele zake na mbele za ulimwengu.

> *2Wakorintho 7:1 "Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu".*

Kumbuka mambo kama haya kuyaondoa, haihitaji kuwa mlegevu legevu, inahitaji kujiingiza wewe mwenyewe katika moto wako, (kujinyima, kukataa na kuepuka) kila kitu ambacho unaona hakimpendezi Mungu. Hata kama nafsi yako inakitamani vipi, unakipinga. Unakubali kuonekana wa ajabu, lakini moyo wako uwe salama, na faida yake utaiona baadaye.

Vilevile hata katika Maisha yetu ya huduma, ili Kristo atende kazi vema, na ukuu wake uthibitike tunapaswa tuondoe mambo yote maovu katikati ya kanisa, tusiwe radhi na wazinzi na wapotoshaji katikati yetu, na Mungu atajifunua miongoni mwetu.

> *Mithali 25:4 “Ondoa takataka katika fedha, Na chombo kitatokea kwa mtakasaji;*
>
> *5 Mwondoe asiye haki mbele ya mfalme, Na kiti chake cha enzi kitathibitika katika haki”.*

Bwana atusaidie sote, Na atubariki.

Shalom.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema,

Kwa maombezi/Ratiba za ibada/ Ushauri/ Maswali.
Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

pia kama utapenda uyapate mafundisho haya kwa njia ya Whatsapp au email basi tutumie ujumbe kwenye namba hizo hizo.

jiunge na channel yetu Kwa kubofya hapa >> WHATSAPP

Mafundisho

Mada Nyinginezo:

> *KUNA UMUHIMU WA KUWA MTU WA KURIDHIKA.*

> *Nini maana ya ombeni kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi wala siku ya sabato?.*

ONDOA TAKATAKA KATIKA FEDHA, NA CHOMBO KITATOKEA KWA MTAKASAJI.

> *Santuri ni nini? (Danieli 3:5,10)*

> *Fuawe ni nini? Kama tunavyosoma katika Isaya 41:7*

> *NYAYO TUNAZOPASWA KUZIFUATA.*

Rudi nyumbani

Share on:
WhatsApp

Print this post